



MUONGOZO WA UTOAJI WA BIDHAA ZA CHAKULA NA VIPODOZI KATIKA VITUO VYA FORODHA KWA BIDHAA ZINAZOSAFIRISHWA BAINA YA TANZANIA BARA NA ZANZIBAR.

1. UTANGULIZI

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi (ZFDA) ni taasisi za serikali zilizoanzishwa chini ya sheria kwa lengo la kusimamia na kudhibiti usalama na ubora wa bidhaa za Chakula na Vipodozi zinazozalishwa nchini na zile zinazotoka nje ya nchi.

Kwa lengo la kurahisisha ufanyaji wa biashara baina ya Tanzania bara na Zanzibar taasisi hizi ziliingia makubaliano mnamo mwaka 2021 katika kusimamia usalama wa chakula na vipodozi ili kutatua changamoto zilizokuwa zikijitokeza katika utekelezaji wa sheria zinazosimamia masuala ya usalama na ubora wa chakula na vipodozi Tanzania.

2. LENGO LA MUONGOZO.

Kuweka utaratibu wa kufuatwa na wafanyabiashara wanaosafirisha bidhaa za Chakula na Vipodozi baina ya pande mbili za Muungano katika vituo vya forodha ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza wakati wa utoaji wa bidhaa hizo.

Aidha muongozo huu utawawezesha wafanyabiashara kufanya shughuli zao bila kuathiri matakwa ya sheria zinazosimamia usalama na ubora wa Chakula na Vipodozi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

3. WIGO WA MUONGOZO

Muongozo huu utahusika na bidhaa za chakula na vipodozi zinazozalishwa ndani na nje ya Tanzania isipokuwa kwa bidhaa ambazo zinalenga makundi yenyе mahitaji maalum ya lishe ikiwemo vyakula nyongeza na fomula za watoto, bidhaa zilizokatazwa au kuzuiwa kisheria na bidhaa zote ambazo huingizwa kwa vibali au ruhusa maalum.

4. UTARATIBU WA UTOAJI WA BIDHAA ZA CHAKULA NA VIPODOZI KATIKA VITUO VYA FORODHA.

4.1. Bidhaa zinazozalishwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

4.1.1. Mfanyabiashara awe na uthibisho wa usajili wa jengo lililosajiliwa na taasisi ya TBS au ZFDA analokwenda kuhifadhiwa bidhaa za chakula na vipodozi.

- 4.1.2. Pamoja na nyaraka za kiforodha za mzigoto mfanyabiashara anatakiwa kuwasilisha cheti cha usajili au leseni ya ubora wa bidhaa kutoka taasisi ya ZFDA au TBS.
- 4.1.3. Kwa bidhaa ambazo hazina ithibati ya ubora, mfanyabiashara anapaswa kuwasilisha cheti cha usajili wa bidhaa na majibu ya vipimo vya maabara yaliyotolewa ndani ya miezi mitatu (3) yanayoendana na mzigoto unaosafirishwa pamoja na kibali cha kusafirisha kilichotolewa na upande husika.

4.2. Bidhaa zinazoingia kutoka nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

- 4.2.1. Mfanyabiashara awe na uthibisho wa usajili wa jengo lililosajiliwa na taasisi ya TBS au ZFDA analokwenda kuhifadhiwa bidhaa za chakula na vipodozi.
- 4.2.2. Pamoja na kukidhi taratibu nyingine za uingizaji wa bidhaa, mfanyabiashara anatakiwa kuwasilisha cheti cha usajili au leseni ya ubora wa bidhaa kutoka taasisi ya ZFDA au TBS.
- 4.2.3. Iwapo aliyesajili bidhaa sie anaesafirisha, anaesafirisha atatakiwa kuwasilisha cheti cha usajili kutoka kwa aliyeisajili pamoja na utambulisho wa ruhusa ya utumiaji wa kibali hicho.